

## TANGAZO

Tunapenda kuwakumbusha wananchi kuwa mfumo wa usajili kwa njia ya Mtandao (ORS) ulionza kutumika tangu tarehe 4 Januari, 2018 ambao pia unaruhusu kutoa huduma zote za baada ya usajili ‘post registration’ za Makampuni kama vile ‘Annual Returns’ na maombi ya mabadiliko yeyote ya Makampuni na Majina ya Biashara kama vile ‘maintenance’ na mabadiliko ya majina n.k. **Huduma hizo sasa zitaanza kutolewa kupitia mfumo wa usajili kwa njia ya Mtandao (ORS) kuanzia tarehe 22 Machi, 2018**, hivyo tunawaomba wamiliki wa Makampuni na Majina ya Biashara wanaohitaji huduma hizo wafuate taratibu za kutumia mfumo wa ORS ikiwa ni pamoja na kuwa na akaunti kwenye mfumo. Ili uweze kuingia kwenye mfumo hakikisha una **Namba ya utambulisho wa Utaifa** kitolewacho na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (**NIDA**). Mfumo unapatikana popote kwa kupitia <https://ors.brela.go.tz/ors> ama tovuti ya BRELA [www.brela.go.tz](http://www.brela.go.tz).

Aidha, Wamiliki wa makampuni wanapaswa kuhakikisha taarifa za makapuni yao zimeingizwa (filing) katika kanzidata ya mfumo wa ORS kwa kupitia kitufe cha ‘*Filing Annuals/Accounts*’ na vivyo hivyo, kwa wamiliki wa Majina ya Biashara watumie kitufe cha ‘*Data Update of existing Business Name*’.